TANGAZO LA SERIKALI NA ..... LA TAREHE .....
SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA NA RASILIMALI ZA ASILI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA, MWAKA 2015

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina.	1.	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira na Rasilimali za Asili) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala za Mwaka 2015.
Matumizi	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lolote chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Tafsiri.	3.	Katika sheria ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo. “Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa mazingira na au Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; ‘Halmashauri’ maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilala; “Hifadhi ya Mazingira’ maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa , viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mhidhiniwa chini ya Sheria ndogo hizi au sheria nyingine yeyote. ‘Kuvuna Misitu’ maana yake ni kufyeka, kukata au kung’oa miti au visiki. “ Maji” maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamiazi mazingira, na ni pamoja na maji ya kunywa ya mito, vijito, maji yanayotiririka,

		yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, bahari, maji yaliyoko chini ya ardhi, na maji yaliyoko katika mkondo. 'Mazao ya misitu' maana yake ni kama ilivyotafsiriwa chini ya kifungu cha 2 cha sheria ya Misitu na nipamoja na kitu chochote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama, majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangwazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la misitu; "Mazingira" maana yake ni masuala yote yanahusisha maumbile halisi ya wazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia Nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibaolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana. "Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishugulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Hamashauri: "Mkurugenzi" maana yake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. "Mifugo" maana yake ni viumbe wanaofugwa na binadamu; "Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 na miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota ua ambayo itajumuisha na yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangaza chini ya sheria za Misitu na mazao yote ya misitu ikijumisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri. "Vitu hatari" maana yake ni vitu vyote vilivyotafsiriwa katika Sheria ua Usimamizi wa Mazingira, ni kemikali yoyote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea, wanyama au viumbe au visivyoonekana na ambavyo ni hatari kwa

		afya ya binadamu, maisha au mazingira; “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. “Mvuvi” maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na shughuli za uvuvi wa samaki na ukusanyaji wa mazao yake. “Kamati ya mazingira” maana yake ni chombo kinachosimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi katika Halmashauri. “Kibali” maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Mkurugenzi kwa mujibu wa sheria ndogo hizi. “Maeneo nyeti” maana yake ni mitelemko ya milima, misitu au maeneo maalumu yaliyotengwa kwa minajili ya misitu au bustani. “Madini” maana yake ni mchanga, kokoto, mawe, udongo, chokaa na mengine yatakayogundulika ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. “Mkaguzi” maana yake ni Afisa mwenye taaluma aliyeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi ya mazingira. “Rasilimali’ maana yake ni kitu chochote cha asili au urithi, au hali yeyote katika Halmashauri. “Kelele“ maana yake kila uchafuzi usababishao na sauti ambao kwa asili unakataliwa au ile iwezao kusababisha athali mbaya kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira pia na pamoja na sauti iwezayo kubainishwa na kamati ya taifa na viwango. “Tathimini ya athari kwa mazingira” maana yake ni uchunguzi wa hatua unaofanywa kubaini iwapo programu, shughuli, au mradi utakuwa na madhara kwenye mazingira. “Ukanda wa kijani” maana yake ni eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi mazingira. “Kamati ya Mazingira” maana yake ni chombo kinachosimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi katika

		Halmashauri. “Maeneo nyeti” maana yake ni miteremko ya Milima, Misitu au maeneo maalumu yaliyotengwa kwa minajiri ya misitu au bustani. “ Mkaguzi” maana yake ni Afisa mwenye taaluma aliyeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi ya ukaguzi wa Mazingira. “Rasirimali za Asili” maana yake ni kitu chochote cha asili (Urithi) au hali yoyote ile katika ardhi ya Halmashauri chenye manufaa kiuchumi na kijamii. “Ukanda wa Kijani” maana yake ni eneo lolote lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuhifadhi mimea ya asili au iliyopandwa kwa madhumuni ya kuhifadhi mazingira.
Wajibu wa Kulinda vyanzo vya maji		**SEHEMU YA PILI** **HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI**
	4. (1)	Halmashauri itawajibika kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.
	(2)	Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji, kuchafua chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.
	(3)	Ni marufuku kwa mtu yeyote, taasisi, kundi la watu au kampuni yeyote kuanzisha na kufanya shughuli za aina yeyote ndani ya mita 60 katika maeneo yote oevu na chepechepe kama vile mto msimbazi na maeneo yote kama Ukanda wa kijani.
Kulinda eneo la hifadhi.	5. (1)	“Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kujenga, kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.
	(2)	Ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu.

	(3)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji cha asili isipokuwa Halmashauri.
	(4)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kuunganisha maji ya mvua na maji taka au kutapisha choo na kutiririsha vinyesi vya mifugo kwenye chanzo cha maji
Uchafuzi wa vyanzo vya maji.	6. (1)	Ni marufuku kwa mtu yeyote, kiwanda, taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.
	(2)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote chenye uhai.
Kuchoma au kusababisha moto		**SEHEMU YA TATU** **HIFADHI YA MISITU**
	7. (1)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma moto kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.
	(2)	Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.
	(3)	Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo na kama atashindwa kushiriki karika zoezi la kuzima moto bila sababu za msingi atakuwa ametenda kosa.
Ukataji miti	8. (1)	Ni marufuku kwa mtu yoyote kukata miti katika eneo la Halmashauri kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali.
	(2)	Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.
	(3)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu

		ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali ya Taifa.
	(4)	Mtu yeyote anaetaka kuvuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa atatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.
Wajibu wa kupanda miti	9.	Kila Mkazi ndani ya eneo la Halmashauri atawajibika:- (a) Kupanda na kutunza miti katika eneo lake; (b) Kupanda na kutunza miti katika makazi yake. (c) Kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomilikiwa.
Ada ya uchafuzi wa mazingira	10.	Mtu yeyote anayeingiza mazao ya misitu katika eneo la Halmashauri anatakiwa kulipa ada ya uchafuzi wa mazingira kama inayoonekana katika jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi.
Uhifadhi wa mazingira ya bahari na udhibiti wa rasilimali zake	11.	**SEHEMU YA NNE** **UHIFADHI WA BAHARI** Ni marufuku kwa:- (a) Mtu yeyote kutumia uvuvi wa juva, baruti, sumu au mkuki; (b) Mtu yeyote kuvulia nyavu ya (“ring net”) kwenye maji mafupi au kwenye miamba. (c) Mtu yeyote kuvua, kuokota, kuchukua au kufanya kitendo chochote kwenye maeneo tengefu ya samaki isipokuwa kwa kibali maalum cha Halmashauri. (d) Mtu yeyote kuvua samaki bila kuwa na leseni ya uvuvi, au (e) Mtu yeyote kutumia chombo cha uvuvi kisichokuwa na namba za usajili pamoja na leseni ya chombo hicho. (f) mtu yeyote kufanya biashara, kupiga picha kwenye ufukwe bila kibali cha Halmashauri.
Udhibiti		**SEHEMU YA TANO** **UHIFADHI WA MAZINGIRA**

wa uchimbaji madini na usafirishaji wake	12.	(1) Ni maarufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini katika eneo la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri. (2) Mtu yeyote aliye na leseni ya uchimbaji madini atalazimika kuomba kibali cha Halmashauri cha kuchimba madini na kukilipia ada kama inavyoelekezwa katika madini na kukilipia ada kama inavyoelekezwa katika Jedwali la Pili la sheria Ndogo hizi. (3) Mtu yoyote atakayesafirisha madini atawajibika kulipa ushuru wa usafirishaji madini kama inavyoelekezwa katika Jedwali la Pili la Sheria ndogo hizi.
Uhifadhi na utunzaji Bustani.	13.	Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara yeyote au kujenga chochote katika eneo la Bustani zote za Halmashauri.
Udhibiti wa ukataji miti na mimea.	14. (1)	Kila mmiliki au anayeishi katika nyumba au anyefanyia biashara atawajibika kupanda miti katika nyumba anayomiliki, anayoishi, anayofanyia biashara inavyofafanuliwa katika jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi
	(2)	Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti isipokuwa kwa kibali cha Mkurugenzi.
Udhibiti wa kelele kwa shughuli mbalimbali za kijamii	15.	Mtu yeyote haruhusiwi kusababisha/kufungulia kelele kupita kiasi iwe muziki, kelele za kiwanda, jenereta au kitu kingine chochote (Sound pollution) bila kupata kibali cha Afisa mhidhiniwa.
Ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira.	16.	Mkurugenzi anaweza kuteua mtu yeyote, taasisi, kikundi binafsi, au asasi ya kiraia, ndani ya Halmashauri katika ngazi ya Mtaa, Kata au Wilaya katika kusimamia uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Tathmini ya athari kwa mazingira na Jamii	17. (1)	Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala haitaendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari za mazingira.
	(2)	Kila mpendekezaji wa Mradi atawajibika kulipa Halmashauri asilimia 10% ya gharama ya tathimini ya athari za Mazingira kama ada ya ukaguzi na usimamizi wa Mradi huu.
Makosa yanayohusu vyanzo vya maji		**SEHEMU YA SITA** **MAKOSA NA ADHABU**
	18.(1)	Mtu yeyote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za hifadhi za vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.
	(2)	Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.
Makosa yanayotokana na uharibifu wa misitu.	19 .	Mtu yoyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:- (a) Atachoma au kusababisha moto misitu bila ya kibali; (b) Atashindwa kushiriki katika kuzima moto: (c) Atavuna mazao ya miti katika misitu isiyohifadhiwa bila kibali; (d) Atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali; (e) Atafyeka nyasi, kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali; (f) Atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au misitu iliyohifadhiwa kama bustani ya mtu. (g) Atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udogo au kinga upepo; (h) Atabandua magome ya miti kwa ajili ya kueneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na vibali; (i) Atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote ziazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.
Makosa yatokanayo na	20.	Mtu yoyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:- (a) Atatumia juva, baruti, sumu au mkuki kuvua;

uharibifu/uchafuzi wa bahari na rasilimali zake.		(b) Atavua kwa kutumia nyavu (ring net) kwenye maji mafupi au kwenye miamba. (c) Atavua, kuokota, kuchukua au kufanya kitendo chochote kwenye maeneo tengefu ya samaki isipokuwa kwa kibali maalumu cha Mkurugenzi. (d) Atavua samaki bila kuwa na leseni ya uvuvi. (e) Atatumia chombo cha uvuvi kisichokuwa na namba za usajili pamoja na leseni ya chombo hicho. (f) Atafanya biashara, kupiga picha kwenye ufukwe bila kibali cha Mkurugenzi.
Makosa yatokanayo na uchimbaji madini na usafirishaji wake.	21. (1)	Mtu yeyote atakua ameteda kosa ikiwa:- (a) Atachimba madini katika eneo la Halmashauri bila kibali cha Mkurugenzi. (b) Atasafirisha madini bila kulipa ushuru. (c) Atasafirisha madini katika vyombo vya usafiri bila kufunika kwa kutumia turubai au gari maalumu la kusafirishia madini.
Adhabu	22.	Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kifungu chochote cha sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa kila kosa au kifungo cha miezi sita jela au vyote faini na kifungo kwa pamoja.
Kufifilisha kosa	23. (1) (2)	Mkurugenzi anaweza kumtoza faini ya shilingi elfu hamsini kwa kila kosa mtu yeyote aliyetenda kosa. Mtu aliyefanya kosa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi atakiri kosa hilo kwa kujaza fomu maalumu na atapewa stakabadhi mara baada ya kulipa faini.
Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 110/2011	24	Sheria Ndogo hizi za (Hifadhi ya mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala za Mwaka 2011 zimefutwa.

JEDWALI LA KWANZA

A: ADA ZA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

(a) Mkaa shilingi elfu mbili (2,000/) kwa gunia.
(b) Mbao shilingi elfu tano (5,000/=) kwa kila ujazo wa mita (1 M^3).
(c) Kuni shilingi elfu tatu (3,000/=) kwa kila ujazo wa mita moja (1M^3).

B: UPANDAJI MITI

Ujazo wa juu .....Miti isiyo pungua 2
Ujazo wa kati .....Miti isiyo pungua 4
Ujazo wa chini.....Miti isiyo pungua 5

JEDWALI LA PILI

ADA YA USAFIRISHAJI MADINI

1. Lori chini ya tani saba (7) .....3,000/=
2. Lori tani saba (7) .....5,000/=
3. Lori zaidi ya tani saba (7).....10,000/=
4. Ada ya uchimbaji madini kwa mwaka .....1,500,000/=

Nembo na mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 03 mwezi Julai, 2015.

.....
Isaya Moses Mngurumi,
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Ilala

.....
Jerry William Silaa
Mstahiki Meya,
Halmashauri ya Manispaa Ilala

NAKUBALI:

.....
Mizengo P. Pinda (MB),
WAZIRI MKUU

DODOMA

Tarehe ...../.....2015